# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA NANE

**15 NOVEMBA, 2018**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA NANE – TAREHE 15 NOVEMBA, 2018

**I. DUA:**

**II. KIAPO CHA UAMINIFU:**

Orodha ya Wabunge wanaoapishwa.

(a) Mhe. James Kinyasi Millya;
(b) Mhe. Joseph Michael Mkundi;
(c) Mhe. Pauline Philipo Gekul; na
(d) Mhe. Ryoba Chacha Marwa.

**III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha za Mwaka 2018 *(The Microfinance Bill, 2018).*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha wa Mwaka 2018 *(The Microfinance Bill, 2018).*

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha wa Mwaka 2018 *(The Microfinance Bill, 2018).*

**IV. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

**V. MASWALI YA KAWAIDA:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**99. MHESHIMIWA GEORGE MALIMA LUBELEJE (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa ina gari moja la kubeba Wagonjwa, gari hilo ni bovu na linahitaji matengenezo makubwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia Hospitali hii magari mawili mapya ili yaweze kutoa huduma ya kubeba Wagonjwa katika Mji wa Mpwapwa na Vitongoji vyake.

**100. MHESHIMIWA MENDRAD LUTENGANO KIGOLA (MUFINDI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Maguvani – Kilolo hadi Udumka.

**101. MHESHIMIWA DKT. MARY MICHAEL NAGU (HANANG'):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wilaya ya Hanang' ina Wafugaji wengi ambao huhama mara kwa mara ili kutafuta malisho na maji na hivyo kuathiri Watoto wao walioko masomoni:-

Je, ni lini Serikali itaunga mkono nguvu za Wananchi katika kujenga Hostel ili kuwasaidia Watoto wa Wafugaji kuendelea na Masomo pindi Wazazi wao wanapohama kutafuta malisho.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**102. MHESHIMIWA JORAM ISMAEL HONGOLI (LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):- Watumishi wa Umma walioajiriwa mwaka 2012 hawajapandishwa madaraja mpaka leo hii:-

Je, ni lini Watumishi hao watapandishwa madaraja.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**103. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM)**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Tabora ni moja ya Mkoa maarufu kwa urinaji wa Asali nchini lakini Warinaji hao bado wameendelea kuwa maskini:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza kwa nini Asali ya Tabora haijaweza kupenya na kupata umaarufu katika soko la Kimataifa;

(b) Aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda alifanya jitihada kubwa ya kuhamasisha Watanzania kufanya ufugaji wa

nyuki; Je, Tanzania inazalisha tani ngapi za Asali na Mkoa wa Tabora unatoa tani ngapi kwa mwaka;

(c) Je, ni lini utaratibu huu wa kununua mazao haya kwa mkopo utaisha.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**104. MHESHIMIWA ESTER ALEXANDER MAHAWE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Tarafa ya Nambis Wilayani Mbulu ina Kata nne (4) na Wakazi 26,000. Pia Tarafa hii ina Shule 5 za Sekondari na Vituo vinne (4) vya Afya lakini haina huduma ya mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya mawasiliano katika Kata hiyo kupitia minara ya simu ili Wananchi wafaidike na huduma hiyo.

**105. MHESHIMIWA VICTOR KILASILE MWAMBALASWA (LUPA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara iliyopewa jina la *"The Great North Road"* hapa nchini ilipitia

njia ya Tunduma, Mbeya, Chunya, Itigi, Manyoni, Singida, Babati Arusha hadi Namanga:-

Je, ni sababu zipi zimefanya Serikali kubadili njia hiyo kupitia GN na kuweka Mbeya, Iringa, Dodoma, Babati, Arusha – Namanga.

**106. MHESHIMIWA DEO KASENYENDA SANGA (MAKAMBAKO)**:

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Baadhi ya Mitaa katika Mji wa Makambako haina mawasiliano; ikiwemo Majengo, Kilimahewa, Lyamkena, Kiumba, Mawade, Kitandililo, Kifumbe, Mahongole, Mlowa na Mkolan'go ambayo ipo umbali wa kilometa 3 – 6 kutoka Mjini:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya mawasiliano katika maeneo hayo.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**107. MHESHIMIWA JOYCE BITTA SOKOMBI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Takribani asimilia 90 ya Jimbo la Musoma Vijijini na Jimbo la Bunda Vijijini hayana

maji safi na salama licha ya Majimbo hayo kuwa kandokando mwa Ziwa Victoria.

Je, ni mkakati gani wa makusudi wa kuhakikisha Mkoa wa Mara hasa Majimbo ya Musoma Vijijini na Bunda Vijijini yanapata maji safi na salama.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**108. MHESHIMIWA ALLY SALEH ALLY (MALINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Chuo cha Diplomasia kimekuwa na umuhimu mkubwa katika masuala ya Kidiplomasia na uwakilishi wa Tanzania nje ya nchi:-

(a) Je, Chuo hicho kimetoa Wahitimu wangapi na mgawanyiko gani hadi sasa;

(b) Je, Wahitimu wangapi hadi sasa wamepanda na kuwa *career diplomats;*

(c) Diplomasia inaenda sambamba na mawasiliano; Je, Serikali haijafikiria kuongeza lugha zinazofundishwa Chuoni hapo.

## VI. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha wa Mwaka 2018 *(The Microfinance Bill, 2018).*

**DODOMA** **S. KAGAIGAI**
**15 NOVEMBA, 2018** **KATIBU WA BUNGE**